TANGAZO LA SERIKALI NA. 944 la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,
(NA. 5 YA MWAKA 2019)

# AGIZO

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.29(1)(d))*

AGIZO LA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA IGUNGA (IGUNGA WSSA), 2019

Jina la Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga(Igunga WSSA), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi), la Mwaka 2019.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2019.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Igunga WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kuanza kutekeleza bei mpya, Igunga WSSA iwasilishe EWURA vielelezokwambailitoataarifakwawateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wananchi, serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma;

(b) Igunga WSSA ihakikishe inanunua na kuweka stoo dira za kutosha kwa ajili ya kubadilisha zilikwisha muda wake ili zoezi la ubadilishwaji wa dira lifanyike kwa kipindi kifupi;

(c) Ifikapo tarehe 31 Januari 2020 au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga itawasilisha EWURA Mpango wake wa

Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(d) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga ihakikishe kuwa inazingatia matakwa ya kukusanya tozo ya udhibiti na kuiwasilisha EWURA;

(e) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga ihakikishe vitabu vyake vya fedha vinakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu ya Serikali au mtu yeyote aliyeidhinishwa kulingana na kifungu 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuwasilisha nakala za mahesabu yaliyokaguliwa EWURA;

Sura ya 348

(f) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili;

(g) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(h) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(i) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA, taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga katika siku zijazo.

Utenguzi wa Agizo Na. 16-017 la mwaka 2016

5. Agizo hili linatengua Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga,(la Bei za Huduma za Maji safi), la Mwaka 2016.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA
BEI NA ADA ZILIZOIDHINISHWA
*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | BeiyaSasa | BeiZinazopendekezwa | | | BeiZilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 855 | 1,131 | 1,311 | 1,381 | 1,060 | 1,060 | 1,060 |
| Taasisi | 1125 | 1,457 | 1,587 | 1,687 | 1,390 | 1,390 | 1,400 |
| Biashara | 1415 | 1,750 | 1,910 | 2,040 | 1,750 | 1,750 | 1,760 |
| Viwanda | 1415 | 1,750 | 1,910 | 2,040 | 1,750 | 1,750 | 1,760 |
| Magati | 1500 | 1,870 | 2,000 | 2,200 | 1,500 | 1,500 | 1,500 |
| WatejawaMajiyaJumla | 3280 | 3,460 | 3,920 | 4,230 | 3,460 | 3,920 | 4,070 |
| BeiyaWastaniLinganisho | 1,041 | 1,340 | 1,508 | 1,605 | 1,244 | 1,248 | 1,251 |

Jedwali Namba 1(b): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada yaSasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | Asilimia 20 yagharamazamaunganisho | Asilimia 20 yagharamazamaunganishonanguvukazikamailivyobainishwakatikakufungu cha 24 KanunizaMajizamwaka 2013. | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |
| Magati | | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada zaSasa | Ada Zinazopendekezwa | | | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 10,000 | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 10,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 10,000 | 10,000 | 20,000 | 20,000 | 10,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 10,000 | 10,000 | 20,000 | 20,000 | 10,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 10,000 | 10,000 | 25,000 | 25,000 | 10,000 | 15,000 | 15,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(f))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| MaelezoyaShughuliZitakazotekelezwa | Kipindi cha Utekelezwaji | | |
|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Kununuadirampya 1041 (zaainayakipenyo cha milimita 20 Daraja C), 302, 413, na 326 kwamwakawa kwanza, pili nawatatusawia | 30.20 | 43.37 | 35.94 |
| Kununuadirazamalipoyakabla 100 zenyekipenyo cha milimita25, daraja C , 30, 30 na 40 kwamwakawa kwanza, pili nawatatusawia | 14.18 | 14.88 | 15.63 |
| Kuongezamtandaowamajikwakilomita 3 wenyekipenyomilimita 100, 75, 63 – 32 bomba la plastiki (uPVC na HDPE) na PN 10 maeneoyaNkonkoto, Hanihani, Mbagala,Masanga, MwayungenaSanzura. | 26.25 | 27.56 | 28.94 |
| Kujengamiundombinuyakuwezakubebatanki la madawa | 5.00 | | |
| Kupataeneo la ekari 10 kwaajiliyakujengamabwawayakutibumaji taka eneo la Hanihani. | | 69.49 | |
| JumlayaGharamazaUwekezaji | 75.63 | 155.30 | 80.51 |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(g))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Kiashiria cha Utendaji | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| NambayaMaunganishomapyayamajisafi | Na. | 302 | 413 | 326 |
| UpotevuwaMaji | % | 27% | 27% | 25% |
| UfanisiwaUkusanyajiwaMapato (bilamalimbikizo) | % | 96% | 97% | 97% |

JEDWALI LA NNE
*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(h))*

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| AINA YA GHARAMA | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
|---|---|---|---|
| UzalishajiMaji | 152.51 | 159.84 | 167.54 |
| UmemekwaAjiliyaUzalishajiMaji | 58.25 | 58.25 | 58.25 |
| UsambazajiMaji | 20.12 | 21.13 | 22.18 |
| Matengenezo | 61.40 | 49.40 | 49.40 |
| Watumishi | 190.84 | 193.60 | 201.70 |
| Utawala | 144.70 | 151.94 | 159.53 |
| Matangazo | 5.03 | 5.28 | 5.55 |
| MatukionaUchangiaji | 2.14 | 2.25 | 2.36 |
| Bodi | 17.18 | 17.38 | 17.59 |
| Fedha | 2.52 | 2.65 | 2.78 |
| JumlayagharamazaUendeshajinaMatengenezo | 654.69 | 661.70 | 686.88 |
| Uchakavu | 103.65 | 103.65 | 98.00 |
| Uwekezaji | 1.82 | 2.09 | 2.22 |
| JumlayaMahitajiyaFedha | 760.16 | 767.45 | 787.10 |
| | | | |
| Ondo Mapatozingine | 15.28 | 22.47 | 18.28 |
| MahitajiyaFedhaKutokaKwenyeMauzoyaMaji | 744.88 | 744.98 | 768.82 |

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*